# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya
Chukwani,Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

## HOTUBA YA KAMATI YA USTAWI WA JAMII YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,**

Awali ya yote natumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia afya njema na kuweza kufika hapa leo hii, kwa lengo la kuwatumikia wananchi wa taifa hili. Aidha, nakupongeza wewe Mheshimiwa Spika kwa jinsi unavyoliongoza Baraza hili kwa ustadi, busara na hekima kubwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Pongezi pia zimwendee Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake mahiri na maono makubwa ya kuiletea Zanzibar maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,**

Shukurani za dhati nazitoa kwa wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa juhudi na umakini wao waliouonesha katika kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii, kwa mwaka wa fedha 2026/2027 na hatimae kuipitisha pamoja na marekebisho madogo madogo waliyoyapendekeza, kwa nia ya kuimarisha zaidi utendaji wa Wizara. Kwa heshima kubwa napenda kuwataja wajumbe hao pamoja na Makatibu wa Kamati yetu kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mheshimiwa Hussein Ibrahim Makungu | Mwenyekiti |
| 2. | Mheshimiwa Nasra Nassor Omar | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub | Mjumbe |
| 4. | Mheshimiwa Issa Ussi Haji (Gavu) | Mjumbe |
| 5. | Mheshimiwa Seif Hamad Suleiman | Mjumbe |
| 6. | Mheshimiwa Shaame Ali Ali | Mjumbe |
| 7. | Mheshimiwa Zainab Khamis Shomari | Mjumbe |
| 8. | Ndugu Mwaka Mwinyi Waziri | Katibu |
| 9. | Ndugu Mussa Issa Mussa | Katibu |
| 10. | Ndugu Moh'd Raymond Mwellu | Afisa Bajeti |

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ya Ustawi wa Jamii imetimiza vyema takwa la kikanuni la kukaa na Wizara na kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka huu wa fedha. Kamati haikuacha kutoa ushauri na maoni kwa yale mapungufu ambayo yamejitokeza katika Makadirio hayo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Afya ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi **6,973,306,000** kutoka katika vyanzo vyake, hadi kufikia mwezi Machi ilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi **4,890,710,000** sawa na asilimia 70.1 ya Makadirio.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza sana Wizara kwa kufikia kiwango kizuri cha makusanyo hayo. Aidha, Kamati inaishauri Wizara kuimarisha usimamizi wa vyanzo vyake ili kuzuia mianya ya upotevu wa mapato hayo, ili nchi iweze kugharamia wenyewe huduma za kijamii zikiwemo huduma za afya.

Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara imekadiriwa kukusanya jumla ya shilingi **9,250,000,000.** Ni imani yetu kwamba Wizara itavuka lengo la ukusanyaji huo.

**Mhsehimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Afya inatekeleza majukumu yake kupitia Programu Kuu Tatu, ambazo ni Programu ya Kinga na Elimu ya Afya, Programu ya Huduma za Tiba na Programu ya Utawala na Uendeshaji. Kiujumla Programu zote hizi zimekadiriwa kutumia jumla ya shilingi **405,890,104,000** kwa kazi za kawaida na kwa kazi za maendeleo.

## PROGRAMU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA

Lengo la Programu hii ni kuhakikisha upatikanaji wa huduma za kinga na kuongeza uelewa kwa jamii juu ya njia mbalimbali za kujikinga na maradhi ya kuambukiza na yale yasiyo ya kuambukiza.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kulifanikisha hili, Kamati inaishauri Wizara ya Afya kuzitekeleza vyema huduma zilizopangwa kutekelezwa, kwa kutoa elimu kwa jamii juu ya kujikinga na maradhi ya kuambukiza na yale yasiyo ya kuambukiza kutokana na athari zake kubwa kwa jamii.

**Mheshimiwa Spika,**

Ni dhahiri kwamba, jamii kubwa imekuwa ikiathirika kwa kiasi kikubwa na maradhi yasiyo ya kuambukiza kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ile ya mitindo ya maisha ambayo jamii kwa sasa inakwenda nayo. Maradhi kama vile ya kansa, presha, sukari yanaendelea kuongezeka kwa kasi visiwani mwetu, hali inayohitaji mashirikiano ya pamoja kati ya jamii na Serikali katika kuliondoa kabisa tatizo hili.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Wizara ya Afya kuendelea na utaratibu wa kuwafanyia wananchi uchunguzi wa mara kwa mara kuhusiana na maradhi kama ya kansa, presha na sukari ili kupunguza au kumaliza kabisa matatizo haya nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Wahudumu wa Afya ya Msingi Ngazi ya Jamii (CHW) ni vijana walioteuliwa na jamii kupitia Shehia zao kwa lengo la kutoa huduma za msingi za afya ndani ya jamii zilizowazunguka. Wahudumu hawa ni uti wa mgongo wa afya za jamii wanajitahidi kutoa huduma za afya kwa jamii zinazowazunguka, lakini Kamati imebaini kuwa, wahudumu hawa maslahi yao ni madogo na hayaendani na kazi kubwa wanazozifanya. Tunaipongeza Serikali kwa nyongeza waliyopatiwa hivi karubuni kutoka posho la shilingi laki moja hadi kufukia laki moja na nusu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, kuwangalia wahudumu hawa kwa jicho la huruma, kuwaongezea posho lao kwa kipindi ambacho wafanyakazi wa Serikali watapatiwa nyongeza za mishahara aliyoitangaza Mheshimiwa Rais katika Madhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani. Ongezeko la posho kwa wahudumu hawa kutaongeza zaidi ari na mori ya kuihudumia jamii iliyowazunguka kwa mapenzi na huruma.

## PROGRAMU YA HUDUMA ZA TIBA

**Mheshimiwa Spika,**

Serikali katika kuhakikisha inaondosha kabisa tatizo la upatikanaji wa huduma za Uchunguzi na Matibabu, imejenga hospitali za kisasa katika kila Wilaya na Mikoa, lakini cha kusikitisha zaidi huduma hizi zinasuasua katika hospitali hizo. Kumejitokeza uzoroteshaji wa upatikanaji wa huduma hizi

kwa wagonjwa wanaofika katika hospitali zetu, jambo linalorudisha nyuma kasi ya Serikali katika kuwaletea wananchi wake maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Wizara ya Afya, kufuatilia kwa karibu utoaji wa huduma katika hospitali hizi, ili kuunga mkono azma na malengo ya Serikali yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inatoa pongezi zake kwa dhati kwa Wakala wa Bohari Kuu ya Dawa kwa kutekeleza vyema majukumu yake ya kutunza na kusambaza dawa na vifaa tiba katika hospitali zote nchini. Kwa sasa Wakala wa Bohari Kuu ya Dawa inakabiliwa na tatizo la ufinyu wa ghala ambalo linatumika katika kuhifadhia dawa na vifaa tiba.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mnasaba huu, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha ujenzi wa ghala la kuhifadhia Dawa na vifaa Tiba Dunga Zuze, ili Wakala wa Bohari wa Dawa waweze kuondokana na changamoto ya kukosa mahala pa kuhifadhia dawa na vifaa tiba pale wanapopata mzigo mkubwa ambao unahitaji kuhifadhiwa kwa wakati mmoja.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, hospitali za Serikali na za binafsi zinapaswa kuwapatia wananchi dawa kwa usahihi wake, kwani kumejitokeza tabia kwa baadhi ya hospitali hasa za binafsi kuwapatia wagonjwa dawa kinyume na maradhi yanayowasumbua, hii inapelekea athari mbaya kwa wagonjwa wanaotumia dawa hizo.

**Mheshimiwa Spika,**

Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ni moja ya nguzo muhimu katika kutoa huduma za kisayansi na kiuchunguzi wa kimaabara kwa taasisi za Serikali kama vile Mahkama na Taasisi za Umma. Vitengo vya ofisi hii kikiwemi Kitengo cha Jinai na Sayansi ya Uchunguzi, Kitengo cha Sumu, Kitengo cha Madawa ya Kulevya, Kitengo cha Chakula na Dawa, Kitengo cha Mazingira, na Kitengo cha Utawala na Mapokezi, vitengo hivyo vinatekeleza majukumu mazito ya kuihudumia jamii.

**Mheshimiwa Spika,**

Wafanyakazi katika kutekeleza majukumu yao hayo wanapaswa kutunza siri za taarifa wanazozifanyia kazi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mnasaba huu, Kamati inaupongeza sana uongozi wote wa Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali Zanzibar, kwa uaminifu wao wanaouonesha katika kutekeleza majukumu mazito waliyokabidhiwa na Serikali. Kupitia hali hii, Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, kuwaongezea maslahi wafanyakazi wa Ofisi hii, ili waweze kuendelea kufanya kazi kwa umakini na kuepuka kurubuniwa na wale wenye madaraka na uwezo wa juu kwa kuwapatia rushwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imebaini kuwa, baadhi ya taasisi za Serikali zinapeleka sampuli katika Maabara hii kwa lengo la kufanyiwa uchunguzi, lakini cha kusikitisha taasisi hizo zinashindwa kulipia gharama za kiuchunguzi kwa sampuli wanazozipeleka. Mfano mzuri ni Jeshi la Polisi. Tukumbuke kwamba, mashine zinazotumika katika kufanyia uchunguzi wa sampuli ni ghali na uchunguzi ni wenye kuchukuwa muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Afya, kuwafuatilia kwa karibu sana wale wote wanaodaiwa na Maabara hii, ili nao waweze kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Afya kuihamasisha jamii kuitumia Maabara hii, kwa kupeleka sampuli za aina tofauti ikiwemo za vyakula, vinasaba, lengo ni kuishi tukiwa salama katika nyanja zote.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa namna ya pekee, sasa nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kuipitia, kuijadili na kuipitisha bajeti ya Wizara hii ili kumuwezesha Mheshimiwa Waziri kutekeleza majukumu aliyajipangia.

**Mheshimiwa Spika,**

Mwisho kabisa, nakushukuru wewe binafsi na wajumbe wako wote kwa kunisikiliza kwa makini wakati nikiwasilisha Makadirio haya. Mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya Kamati yangu naunga mkono hoja kwa asilimia moja.

Ahsante sana

……………………

Hussein Ibrahim Makungu,

Mwenyekiti,

Kamati ya Ustawi wa Jamii,

Baraza la Wawakilishi,

**<u>Zanzibar.</u>**